**MKATABA WA KUPANGISHANA SHELI**

**KATI YA**

**BW: BAHATI MSAJIE MNOZYA**
**PAMOJA NA**
**BI: ANETH JOSEPH MWAKINDU**
**WA S.L.P 132,**
**TUNDUMA**
**(WAPANGISHAJI)**

**NA**

**MANYANYA OIL LIMITED**
**S.L.P 132,**
**TUNDUMA.**
**(MPANGAJI)**

**KATIKA SHELI ILIYOPO KATIKA ENEO LILILOPIMWA LIJULIKANALO KAMA PLOT NO. 18 Block "H" TUNDUMA MJINI, MTAA WA POLICE, KATA YA TUNDUMA KATIKA WILAYA YA MOMBA MKOA WA SONGWE.**

NEEMA SARUNI
Advocate,
Notary Public
&
Commissioner
for Oaths
P.O. Box 162, Tunduma, Tanzania

Scanned with CamScanner

**MKATABA** huu umefanyika leo tarehe 21 mwezi wa 01 mwaka 2023.

kati ya

**BAHATI MSAJIE MNOZYA PAMOJA NA ANETH JOSEPH MWAKINDU** wa Sanduku la Posta 132 TUNDUMA kwa upande mmoja (ambao katika mkataba huu wataitwa **"WAPANGISHAJI"**),

NA

**MANYANYA OIL LIMITED** ambayo ni kampuni iliyosajiliwa nchini Tanzania kwa mujibu wa sheria ya makampuni ya mwaka 2002 ya sanduku la posta 132 TUNDUMA ambayo katika mkataba huu itaitwa **"MPANGAJI"**.

KWA KUWA Wapangishaji ni wamiliki halali wa SHELI iliyopo katika eneo tajwa hapo juu katika sheria halali za upangishaji, hivyo watampangisha mpangaji kwa kipindi kitakachokubalika ndani ya miaka mitano tu.

KWA KUWA mpangaji amemwendea wapangishaji wa SHELI kwa nia ya kutaka kupanga sheli hiyo kwa malipo ya kodi iliyokubaliwa katika mkataba huu na kwa mujibu wa masharti mengineyo yatakayoafikiwa kwenye mkataba huu.
KWA KUWA mwenye sheli amekubali kumpangisha mpangaji katika sheli hiyo;

**HIVYO BASI, MKATABA** huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo:-

1. KWAMBA Wenye sheli wamempangisha mpangaji sheli hiyo iliyopo katika eneo lililotajwa hapo juu kwa kiasi cha kodi ya shillingi MILLIONI MOJA NA LAKI TANO TU (Tshs 1,500,000/=) kwa mwezi.

2. KWAMBA pesa hiyo ya pango itakuwa inalipwa kila mwezi na mkataba huu utakuwa ni wa miaka mitano tu kuanzia leo tarehe 21/01/2023 mpaka 21/01/2029 ambapo leo siku ya kusaini mkataba huu kitalipwa kiasi cha shillingi millioni **MOJA NA LAKI TANO TU (tshs 1,500,000/=)** ambayo itakuwa ni pesa ya kodi kuanzia tarehe 21/01/2023 na kuisha tarehe 21/01/2024.

3. KWAMBA, MPANGAJI atatakiwa kutunza mali zote za WAPANGISHAJI zilizopo katika sheli hiyo na baada ya makataba kuisha MPANGAJI atatakiwa kuwakabidhi WAPANGISHAJI mali zote kama zilivyo kabidhiwa.

4. KWAMBA, ikiwa Mpangaji anatimiza masharti yote ya ulipaji kodi na mengineyo, Wapangishaji wanampangisha mpangaji sheli hiyo bila kumuingilia katika kipindi chote cha upangaji huo isipokuwa pale itakapo lazimu tu.

5. KWAMBA Mpangaji anatakiwa azingatie usafi wa sheli pamoja na mazingira yake na anatakiwa atumie sheli hiyo kwa matumizi ya biashara tu na sio vinginevyo na yote haya yanafanyika pasipo kufanya



NEEMA SARUNI Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths P.O. Box 162, Tunduma Tanzania

Scanned with CamScanner

shughuli nyingine yoyote tofauti na iliyokusudiwa katika sheli hiyo ambacho kitakuwa ni kinyume cha sheria na taratibu za nchi.

6. KWAMBA wapangishaji, kwa wakati muafaka wanayo haki ya kuingia katika sheli hiyo pale inapobidi ili kukagua au kufanya ukarabati wa sheli hiyo au kuchunguza endapo kuna dosari yoyote iliyojificha. Hivyo mpangaji atataarifiwa kuhusu hilo na kwamba ni vizuri iwe katika masaa ya kazi.

7. KWAMBA Mpangaji anatakiwa aiweke sheli hiyo anayopanga katika hali ya usafi wakati wote na kuhakikisha kwamba kuta na sehemu zingine za sheli haziharibiwi.

8. KWAMBA Mpangaji anatakiwa alipie gharama zote zitakazojitokeza katika upangaji wake ambazo zinahusiana na biashara yake. mfano, maji, umeme au simu katika sheli hiyo kwa muda wote atakaopanga sheli hiyo na wakati wa kuondoka katika sheli hiyo atahakikisha kuwa hataacha madeni yoyote yanayohusiana na umeme, maji au simu.

9. KWAMBA Mpangaji haruhusiwi kufanya matengenezo au marekebisho yoyote katika sheli hiyo aliyopanga bila idhini ya maandishi kutoka kwa Wapangishaji,

10. KWAMBA Mpangaji haruhisiwi kukodisha mtu au mfanya biashara mwingine, au mtu mwingine sheli hiyo aliyopanga kwa mtu mwingine yeyote bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa Wapangishaji, na ikiwa Mpangaji atashindwa kuendelea na Mkataba basi mpangaji atamrudishia sheli kwa mwenye nyumba na kukabidhiana kwa maandishi kama ilivyokua wakati wa kuingia.

11. KWAMBA Mpangaji amjulishe wapangishaji wa sheli kwa maandishi mwanzo wa miezi miwili ya mwisho ya mkataba huu endapo atapenda kuendelea na mkataba huu mara utakapokwisha.Tofauti na hapo itaonyesha kuwa mpangaji hatarajii kuendelea na upangaji.

12. KWAMBA Mpangaji na wapangishaji wanaweza, na wote wana haki ya kusitisha mkataba huu kwa kutoa taarifa kwa maandishi miezi miwili kabla. Endapo kutahitajika majadiliano yoyote kuhusu hili, basi mpangaji na wapangishaji watajadili. Hata hivyo makubaliano yote yatakuwa yakiongozwa na mkataba huu.

**<u>HAKI ZA MPANGAJI</u>:**

13. Mpangaji anahaki ya kuendesha biashara yake bila kubughudhiwa pasipo lazima isipokuwa tu pale ambapo mpangaji atavunja masharti muhimu ya mkataba huu.
14. Mpangaji anahaki ya kuwa huru na kutoingiliwa katika biashara yake ila pale tu atakapogeuza matumizi halali ya sheli kwa matumizi yake binafsi kinyume na makubaliano
15. Mpangaji anahaki ya kuwaita wapangishaji na kujadili nao masuala yoyote yanayohusiana na sheli katika hali ya ustaarabu na heshima na si vinginevyo.

NEEMA SARUNI
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
P.O. Box 162



Scanned with CamScanner

16. Mpangaji anahaki ya kupata taarifa yoyote ile muhimu kuhusiana na upangaji na biashara yake pindi itakapohitajika na kwamba pawepo na mawasiliano mazuri kati ya mpangaji na wapangishaji.

**KWA USHUHUDA** na **UTHIBITISHO**, mkataba huu umewekwa sahihi na Wapangishaji na mpangaji kama inavyoonyeshwa hapa chini:

IMETIWA SAHIHI hapa Tunduma na
**BAHATI MSAJIE MNOZYA**
Aliyetambulishwa kwangu na
..........................................
LEOTarehe..21..mwezi..01....mwaka 2023

MPANGISHAJI WA KWANZA

IMETIWA SAHIHI hapa Tunduma na
**ANETH JOSEPH MWAKINDU**
Aliyetambulishwa kwangu na
..........................................
LEOTarehe..21..mwezi....01...mwaka2023

MPANGISHAJI WA PILI

MBELE YANGU:
Jina ...NEEMA SARUNI..........

Sahihi..........

Anuani....S.L.P 162 TUNDUMA....

Wadhifa ....WAKILI.......

NEEMA SARUNI Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths P.O. Box 162, Tunduma-Songwe Tanzania

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI
WA KAMPUNI YA **MANYANYA OIL LIMITED**
**IKIWAKILISHWA NA**
ANETH MWAKINDU
Ninayemfahamu Binafsi
LEO Tarehe..21...mwezi.01..mwaka, 2023

MPANGAJI

MBELE YANGU:
Jina ...NEEMA SARUNI..........

Sahihi..........

Anuani....S.L.P 162 TUNDUMA....

Wadhifa ....WAKILI.......

NEEMA SARUNI Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths P.O. Box 162, Tunduma-Songwe Tanzania



Scanned with CamScanner